Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

# Mitazamo ya Walimu wa Fasihi ya Kiswahili Kuhusu Ufaafu wa Hadithi Fupi Teule kwa Bibliotherapia.

**Rose Mavisi[1]; Dr. Gwachi Mayaka[2]; Prof. Wendo Nabea[3]**
**Laikipia University, Kenya.**
**Main author email: rosemasai@gmail.com**

## IKISIRI

Makala haya yalilenga kutathmini mitazamo ya walimu wa fasihi kuhusu ufaafu wa hadithi fupi kutumika kama bibliotherapia ya matatizo yanayowakumba wanafunzi. Utafiti huu ulipata matini yake kutoka kwa hadithi fupi teule zifuatazo; *Mayai Waziri wa Maradhi na hadithi nyingine* (2004), *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Kiti cha Moyoni na hadithi nyingine* (2007) na *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* (2016). Mwalimu alifaa kuteua hadithi mwafaka kwa mwanafunzi kwa kuzingatia umri, maudhui yanayojitokeza na usawiri wa wahusika waliopitia matatizo yaliyo sawa na yale ya wanafunzi husika. Mbinu iliyotumiwa kukusanya data hii ni hojaji wazi na funge. Mtafiti aliwahoji walimu wa fasihi ya Kiswahili katika shule za upili Kaunti ya Nairobi. Mtafiti alitumia seti mbili za hojaji kama vifaa vya kukusanya data ya walimu. Hojaji zilizotolewa kwa walimu ishirini na wanane zilikuwa na maswali funge na huru. Maswali funge yalikuwa na muundo maalum ili kumpa mtafiti nafasi ya kupata majibu yasiyo na maelezo ya ndani. Maswali huru yalimpa mtafiti uwezo wa kupata data yenye undani kuhusu mitazamo ya walimu wa fasihi ya Kiswahili kuhusu matumizi ya hadithi fupi teule za Kiswahili kama bibliotherapia kwa wanafunzi. Nadharia ya NMMM yake Rosenblatt (1995) ilitumika katika kuchanganuakazi hii.

**Maneno muhimu**: Bibliotherapia, mitazamo, walimu, hadithi fupi.

---***---
**How to cite this article in APA (6th Edition)**
Mavisi, R., Mayaka, G. & Nabea, W. (2021). Mitazamo ya Walimu wa Fasihi ya Kiswahili Kuhusu Ufaafu wa Hadithi Fupi Teule kwa Bibliotherapia. *Editon Cons. J. Kiswahili,* 3(1), 254-275. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v3i1.228
---***---



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

**Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)**

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

## UTANGULIZI

Matumizi ya bibliotherapia darasani humpa mwanafunzi nafasi ya kukabiliana na matatizo yake katika mazingira salama. Walimu wanastahili kukuza uhusiano mzuri wa uaminifu na wanafunzi wao. Hivyo wanafunzi watakuwa wazi kuelezea yale wanayopitia kwa mtu wanayemuamini. Mwalimu anafaa kutafiti ili ateue kitabu mwafaka kwa huyu mwanafunzi kwa kuzingatia umri, uwezo wa kusoma, maudhui yanayojitokeza na usawiri wa wahusika wanaopitia matatizo yaliyo sawa na yale ya wanafunzi husika. Mwalimu ateue njia mwafaka za kuanzisha usomaji wa kitabu kilichoteuliwa. Usomaji uanzie juu ya jalada hadi kwa yaliyo ndani. Wanafunzi waongozwe na mwalimu katika usomaji wa matini ya BB. Hii itategemea kama ni mmoja au kundi dogo la wanafunzi. Ajadili msamiati unaoonekana mpya na pia kuwauliza maswali kuhusiana na kitabu husika. Kulingana na Maich na Kean (2004), kitabu kinachoteuliwa kwa BB kinafaa kuwa na hadithi sahili inayoeleweka na kuaminika. Hadithi hii yafaa kutosheleza hisia, mahitaji na malengo ya wanafunzi. Aidha, inafaa kuangazia tamaduni mbalimbali, usawa wa kijinsia na hali ya kuwa bila vurugu. Mwandishi hupaswa kuwasawiri wahusika wanaoweza kusuluhisha matatizo yao. Kupitia usomaji wa hadithi, wanafunzi watajifunza kupitia uhusiano wao na wahusika jinsi wanavyoweza kukabiliana na hali zao mbalimbali maishani.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Bibliotherapia na Mitazamo ya Walimu kuhusu Ufaafu wa Hadithi fupi

Dawn (2020), alieleza jinsi walimu walitumia bibliotherapia kama mbinu ya kufunzia ili waweze kuelewa tabia za wanafunzi wa kiwango cha gredi ya tatu hadi tano. Walimu walidhamiria kuchunguza ikiwa usomaji kwa sauti kwa wanafunzi unaweza kuwasaidia kuelewa masomo pale darasani. Sampuli ya utafiti ilihusisha walimu kumi wanaofundisha gredi ya tatu hadi tano katika wilaya ya Florida kusini. Mbinu za kukusanya data zilihusisha hojaji, mahojiano na kundi lengani. Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo: Ni vipi walimu huelezea kusoma kwa sauti kwa misingi ya kibibliotherapia darasani? Pili walimu wana mtazamo upi kuhusu kusoma kwa sauti darasani kama mbinu ya kujifunza ili waweze kuyaelewa yaliyomo? Tatu, walimu wana mtazamo kuhusu kusoma kwa sauti kama njia ya kubadili tabia ya wanafunzi darasani? Data iliyochanganuliwa ilihusisha baadhi ya mada yafuatayo: mahitaji ya wanafunzi, ushirikiano, kujitambulisha na wahusika vitabuni mwingiliano wa wanafunzi, ushiriki wa wanafunzi, ufundishaji uliongozwa na mwalimu na uhalisia wa kimaisha. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa usomaji kwa sauti darasani huweza kuimarisha matokeo ya wanafunzi hao darasani hivyo kutimiza bibliotherapia darasani. Utafiti huu ulirutubisha wetu kwani mbinu za kukusanya zinazotumika zilisaidia katika kuimarisha utafiti wetu na vile vile mandhari ambapo tafiti zote mbili zinatendeka ni darasani. Tofauti ni kuwa tuliangazia tathmini ya bibliotherapia darasani tukimlenga mwalimu ilhali utafiti huu unashughulikia wanafunzi kusoma kwa sauti darasani. Utafiti huu pia ulishughulikia iwapo usomaji kwa sauti unaweza kubadili tabia za wanafunzi ilhali wetu ulishughulikia iwapo vitabu vya hadithi fupi vilivyoteuliwa vina wahusika ambao wanafunzi wanaweza kuwaiga ili kubadili tabia na mitazamo yao kuhusu maisha. Zaidi utafiti wao ulishughulikia wanafunzi wa gredi za chini ilhali wetu ulishughulikia wanafunzi wa gredi za juu ambao wanafunzwa fasihi kama somo la kutahiniwa.

Doss (2010), alibaini jinsi mikakati ya kibibliotherapia iliweza kuathiri mitazamo ya walimu kuhusu tabia za uchokozi za wanafunzi wao. Matokeo ya utafiti yalifichua kuwa hata wanafunzi wa umri wa miaka minne na mitano huwachokoza wenzao darasani. Mitazamo ya walimu



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kuhusu wanafunzi hawa na uchokozi darasani inabadilika. Utafiti huu ulirutubisha wetu kupitia matumizi ya kundi lengani. Utafiti wetu ni tofauti kwani uliangazia mitazamo ya walimu kuhusu ufaafu wa hadithi fupi kwa BB kwa kutathmini mitazamo ya walimu kuhusu ufaafu wa wahusika wanaoaminika, wahusika ambao wanazingatia usawa wa kijinsia, jinsi wahusika wanavyosuluhisha matatizo yao, umri wa wahusika na iwapo wanafunzi wanaweza kubadili mitazamo yao kuhusu maisha baada ya kusoma hadithi fupi.

Wilson (2014) alizungumzia warsha ya bibliotherapia iliyoandaliwa ili kuwasaidia walimu walio mafunzoni kubadili mtazamo wao hasi kuhusu somo la hisabati. Katika warsha hii walimu walijipanga katika vikundi vidogo vidogo ili kujadili kuhusu matatizo waliyopitia waliposoma somo hili na walipojiandaa vyuoni ili kuwafundisha wanafunzi. Warsha hii ilihusisha mtafiti, mshauri wa wanafunzi na walimu walio chuoni. Katika makundi yao waliandika juu ya visa muhimu katika ujifunzaji wao wa hisabati na vile vile kuhusu tafakari zao. Uzoefu wao uliangazia wasiwasi waliopitia kuhusu somo la hisabati. Majadiliano hayo yaliangazia hitaji la mwamko wa wakufunzi wa walimu vyuoni juu ya mitazamo yao kuhusu somo la hisabati. Utafiti huu ulirutubisha wetu kwani matumizi ya kundi lengani ili kupata data husika ilitusaidia katika mijadala ya wanafunzi kuhusu sifa za kibiliotherapia katika haditi fupi teule. Katika utafiti wa Wilson aliangazia matatizo ambayo walimu waliyapitia waliposoma somo la hisabati. Tofauti na utafiti wetu ambao ulitathmini mitazamo ya walimu wa fasihi kuhusu jinsi hadithi fupi zinaangazia matatizo ambayo yanawakabili wanafunzi na suluhu ambazo zinatolewa kupitia wahusika ili kubaini iwapo zinafaa kutumika kama BB.

Utafiti wa Lutovac na Kaasila (2011) ulimlenga mwalimu kwa jina Ulla, ambaye alishikilia hisia hasi katika somo la hisabati, lakini kupitia bibliotherapia alilegeza mtazamo wake hasi wa hisabati na kugundua kuwa angefurahi kufundisha hisabati kwa kushiriki na kutafakari juu yake mapema. Fasihi kwa sasa haina habari ya kutosha juu ya jinsi walimu wanavyotambua bibliotherapia kama mkakati wa kufundishia katika mazingira ya darasani, hasa linapokuja suala la kuitumia kama zana ya kuwasaidia walimu katika kushughulikia masuala yasiyokuwa ya kielimu ambayo watoto na vijana wanakabiliwa nayo. Pengo hili katika fasihi ni shida na ni kizuizi cha utekelezaji mzuri wa bibliotherapia shuleni. Utafiti huo ni wa kwanza wa aina yake na unakusudia kutoa kwa utaratibu maoni ya wanafunzi wengine wa shahada ya kwanza waliyoshikilia kuhusu bibliotherapia na utekelezaji wake kama zana ya kufundishia kwa watoto na vijana katika mipangilio ya shule. Utafiti huu ulikuwa ni rutubisho kwa utafiti wetu ambao uliangazia mitazamo ya walimu kuhusu matumizi ya bibliotherapia katika darasa la fasihi.

Kulingana na Dobyns (2015), watoto wenye ulemavu hawashirikishwi sana kwenye shughuli za pamoja kama vile michezo wakati wanapopumzika, kwa sababu ya kutengwa na wengine. Watoto wasio na ulemavu mara nyingi hawatambui au hawaelewi udhaifu wa watoto walemavu na hivyo basi ni nadra sana wawakubali na hali zao. Matini za bibliotherapia zimetumika kwa muda mrefu kufunza kuhusu hali ngumu kwa kuwahamasisha wanafunzi kujenga mahusiano ya kibinafsi na wahusika katika vitabu na hivyo basi unawawezesha wasomaji kutathmini tabia na hisia zao kupitia uzoefu wao na wahusika katika hadithi (Rozalsks na wenzake, 2010). Hata hivyo, kuna tafiti chache sana kuhusu bibliotherapia ya watoto. Maoni ya walimu yalitusaidia katika kutathmni iwapo vitabu vya HF vinazingitia watoto walemavu.

McCulliss (2012) anadai kuwa nyenzo za therapia burudani zinataja bibliotherapia katika vitabu vingi na



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

mitandaoni lakini kuna makala machache sana ya utafiti kuhusu matumizi ya bibliotherapia na wanatherapia burudani. Mwanya huu wa utafiti ndio uliochochea utafiti wetu. Licha ya kuwa kundi lililolengwa lilikuwa la vijana na si watoto, matokeo ya utafiti huu hayajatiliwa shaka. Ikiwa usomaji unashirikishwa na mchakato au uchambuzi kama ilivyo katika bibliotherapia, utafiti umedhihirisha matokeo mazuri zaidi katika hisia, ushirikiano na kiakili (McCulliss, na Chamberlain, 2013). Manufaa ya kijumla yanajumlisha kujengeka kwa kujithamini, kuboreka kwa umakinifu, kujiamini, kujieleza, kutambua namna ya kutatua matatizo, uvumilivu wa matatizo, uwezo wa kuratibu mazoea ili kujenga uelewaji, kuelewa maamuzi na mawazo sahihi. Matokeo ya kihisia yanahusu kujenga umakinifu, kuwa na huruma, kubadili mitazamo na kupunguza lawama, huzuni na wasiwasi kijitetea, kupunguza hali ya kuwa hoi, kuwa salama na kuepuka uchokozi, kupunguza msongo, kukubali mazoea na hisia, na kujithamini (Steward, na Ames, 2014). Licha ya kwamba wanafunzi wanasoma ili kupita mtihani, suala hili lilikuwa muhimu ili kutathmini maoni ya walimu kuhusu hadithi fupi ambazo zinaweza kuwa na vipengele kama hivi na ambazo zinaweza kutumika kama BB.

Wilson na wenzake (2013) anaeleza kuwa uwezo wa walimu walio mafunzoni kabla ya kufuzu kushiriki vizuri katika somo la hisabati huwa ni mkakati muhimu kwa kuzalisha raia ambao wanaweza kutumia hisabati vyema katika maisha yao. Walimu hawa wanaweza kuwa na wasiwasi kwa somo la hisabati hivyo kuathirika katika ufundishaji wa siku zijazo wa hisabati. Utafiti huu uliwalenga walimu mia mbili na kumi na tisa wanaoanza kozi ya ualimu katika chuo kikuu cha Australia. Ilibainika kuwa walimu hawa wanapokuwa mafunzoni hukumbwa na wasiwasi mkubwa kuhusu somo la hisabati hivyo kuathiri ufunzaji wao pamoja na wanafunzi wanaowafundisha kuwa na mtazamo hasi kuhusu somo hili. Bibliotherapia ilitumiwa kama mkakati wa kuwasaidia walimu hao. Utafiti huu ulibaini mitazamo hasi ya walimu wakiwa mafunzoni kuhusu somo la hisabati ilivyoathiri ufunzaji wao kuhusu somo hili. Tofauti na utafiti huu ambao tulichunguza mitazamo ya walimu kuhusu ufaafu wa hadithi fupi kutumika kama BB darasani. Ni wazi kwamba watafiti wengi wanaegemea kuhusu mitazamo ya walimu kuhusu somo la hisabiti, utafiti huu uliegemea somo la fasihi hasa mitazamo ya walimu wa fasihi kuhusu ufaafu wa hadithi fupi kama bibliotherapia.

## MATOKEO

Sehemu hii ilitathmini majibu ya walimu katika hojaji funge na huru kuhusu ufaafu na ufanisi wa hadithi fupi kwa bibliotherapia. Nadharia ya NMMM yake Rosenblatt (1995) ilitumika. Katika kuchanganua hojaji huru kati ya mtafiti na walimu. Mbinu ya usimbaji ilitumika katika hojaji huru. Maana ya alama hizi za usimbaji ni; mwalimu **(MW)** shule za kitaifa **(KI)** kaunti **(KA)** kaunti ndogo **(KN)** na za wilaya **(W).** Jedwali lifuatalo linaonyesha majibu ya walimu hawa.

**Jedwali la Mitazamo ya Walimu wa Fasihi Kuhusu Ufaafu wa HF teule kama BB**

| | Nakubali Kabisa | | Nakubali | | Sina Uhakika | | Sikubali | | Sikubali Kabisa | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | idadi | % | idadi | % | Idadi | % | idadi | % | idadi | % |



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **HF inasawiri matatizo yanayowakabili wanafunzi wa shule za upili** | 28 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **HF ina wahusika wanaopata suluhu kwa matatizo yao.** | 3 | 11 | 7 | 25 | 0 | 0 | 18 | 64 | 0 | 0 |
| **HF inasawiri wahusika wanaoaminik kwa wanafunzi** | 8 | 29 | 14 | 50 | 2 | 7 | 4 | 14 | 0 | 0 |
| **HF inampa mwanafunzi uwezo wa kujithamini** | 22 | 79 | 4 | 14 | 0 | 0 | 2 | 7 | 0 | 0 |
| **HF inasawiri wahusika wanaoweza kuwasaidia wanafunzi kubadili mitazamo yao kimaisha** | 10 | 36 | 0 | 0 | 0 | 0 | 18 | 64 | 0 | 0 |
| **HF inasawiri wahusika wa kuigwa na wanafunzi** | 16 | 57 | 5 | 18 | 0 | 0 | 7 | 25 | 0 | 0 |
| **HF inaangazia wahusika walio na usawa wa kijinsia** | 14 | 50 | 10 | 36 | 0 | 0 | 4 | 14 | 0 | 0 |
| | | | | | | | | | | |
| **HF inafaa ilenge wanafunzi kiumri** | 19 | 68 | 0 | 0 | 7 | 25 | 2 | 7 | 0 | 0 |

Jedwali hili **linaonyesha** matokeo ya kutathmini mitazamo ya walimu wa fasihi kuhusu ufaafu wa hadithi fupi kutumika kwa bibliotherapia. Walimu ishirini na wanane walijaza hojaji kwa kutumia vigezo vitano vya likati ili kuonyesha mitazamo yao kuhusu bibliotherapia; nakubali kabisa, nakubali, sina uhakika, sikubali na sikubali kabisa. Walimu walipojaza hojaji hizi walikuwa huru kutoa maelezo ya majibu yao kupitia hojaji huru.

**a) Matatizo Yanayowakumba Wanafunzi**

Matumizi ya BB yanapaswa kudhihirisha changamoto zinazowakumba wanafunzi katika maisha yao. Hali hii itawasaidia kukabiliana na tatizo hilo bayana. Katika utafiti huu, tulitaka kujua mitazamo ya walimu kuhusu iwapo HF zilizingatia matatizo yanayowakumba wanafunzi kama mojawapo wa kipengele cha bibliotherapia. Kwa mujibu wa data hii, asilimia 100ya walimu walikubaliana sana kwamba HF teule zilisawiri



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

matatizo yaliyowakabili wanafunzi katika maisha yao. Kauli za walimu hawa zilielezwa kupitia hojaji huru. Mwalimu **MW$_1$KI** alisema yafuatayo:

> *Matumizi ya mihadarati katika jamii ni tatizo ambalo limeibuka katika jamii zetu.Hili ni tatizo ambalo huwaathiri wanafunzi wengi wa shule za upili wasichana kwa wavulana. Walimu katika shule hizi wanatafuta njia ya kuweza kukabiliana na tatizo hili. Taswira hii inajitokeza kupitia mhusika Nanda katika hadithi ya* ***Fumbo la Mwana.*** *Aliingilia matumizi ya mihadarati ambayo yalimwathiri kiafya na hata kimasomo. HF hii inasawiri tatizo la wanafunzi kutumia mihadarati.*

Matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili na msingi yamekithiri ni visa ambavyo vimeripotiwa mara kwa mara hapa nchini Kenya. Usomaji wa hadithi hii unaweza kuwafungua macho wanafunzi ambao wangali usingizini ili waweze kujiepusha na uraibu wa aina hii na kuwahadharisha wengine ambao wangeishia katika mkondo huo. Ufahamu pia unaweza kuelezewa kama hatua ya kufikia kujitambua kupitia fasihi kwa maisha yao wenyewe. Watoto na vijana wanaweza kutumia ufahamu mpya uliopatikana kubadili tabia zao na kujibu kwa ukomavu zaidi wanapokabiliwa na changamoto (Turner, 2004).Wanafunzi hawa pia hutambua kuwa wao si wa kwanza kushiriki uraibu wa aina hii. Kwa hivyo, Taasisi ya Ukuzaji Mitaala nchini (KICD) inapoteua vitabu inafaa kuzingatia uteuzi wa hadithi fupi ambazo zina wahusika ambao wanafunzi wanaweza kujinasibisha nao ili waweze kutatua baadhi ya matatizo wanayopitia**.** Pia mtaala wa elimu unapaswa kuhusisha bibliotherapia katika usomaji wa hadithi fupi ili kujenga uhusiano kati ya mwanafunzi na wahusika. Ni muhimu ikiwa wanafunzi wataingiliana na wahusika inavyotakikana ili mfumo huu ufanikiwe. Hatua ya utambuzi ya matatizo yanayowakumba wanafunzi inapaswa kuzingatiwa wanapoteua hadithi fupi ili wanafunzi waweze kutambua na kujihusisha na wengine wanaopitia hali kama zao au wanaoakisi hali zao.

Naye mwalimu **MW9KA** alieleza kuwa:

> *Baadhi ya wanafunzi katika shule za upili na msingi hushiriki mapenzi wakiwa shuleni na wengi huishia kuwa waja wazito. Visa vingi vya wanafunzi kupata mimba vimeripotiwa kutoka Kaunti mbalimbali nchini Kenya. HF ya* ***Kanda la Usufi*** *imesawiri haya kupitia Sela na Masazu ambao walishiriki mapenzi wakiwa shuleni. Sela alipata mimba na kulazimika kuacha shule. HF hii inaonyesha hali halisi iliyopo katika jamii. Haya ni baadhi ya matatizo ambayo wanafunzi hukumbana nayo.*

Tatizo la wanafunzi kushiriki mapenzi wakiwa shuleni limekuwepo tangu jadi. Wanafunzi wengi huishia kuacha shule baada ya kuwa wajawazito. Hata hivyo, serikali imefanya juhudi kuwapa wanafunzi hasa wa kike nafasi ya kuendelea na masomo baada ya kujifungua. Katika kipindi cha ugonjwa wa korona, visa vya wanafunzi nchini kuwa wajawazito viliongezeka sana. Huenda hili lilitokana na sababu kwamba wanafunzi hawa hawakuwa shuleni kwa hivyo hawakupata usaidizi wa vitu vingine kama vitambaa vya sodo walivyokuwa wakipewa shuleni na pengine hili liliwatia katika kishawishi cha kushirikiana kimapenzi na wanaume waliowaahidi vitu hivi. Hadithi ambazo zinaangazia masuala ya mimba za mapema zinapaswa kupewa kipaumbele na KICD ili wanafunzi wajifunze kutokana nazo. Walimu wa fasihi wanapaswa kufunzwa vyuoni namna ya kutumia bibliotherapia katika kuchambua hadithi fupi ili kutambua masuala ya wanafunzi wao, kushughulikia masuala ya kijamii na



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

kihisia kabla hayajatokea; na kuwapa mwelekeo wa siku za usoni kwa mifano ya jinsi wahusika walivyoweza kushughulikia hali sawa na hizo. Walimu wanapofunza pia hawapaswi kuwakemea wanafunzi ambao wamepata watoto wakiwa shuleni hasa jinsia ya kike. Hadithi hizi pia zinapaswa ziangazie njia mwafaka za kusuluhisha masuala ya ujauzito. Jinsia ya kiume nayo inapaswa idhihirishiwe kwamba kupachika wasichana mimba lazima wataubeba huo mzigo bega kwa bega sio kuachiwa tu msichana. Kwa hivyo, hadithi fupi ziwe na wahusika ambao wataelimisha wanafunzi kuhusu utata wa ujauzito wakiwa bado shuleni. Wanafunzi wakisoma hadithi kama hii watajua kuwa wao si wa kwanza kupitia hali kama hii. Usomaji kwa jumla umesaidia watoto na hata vijana kubaini hisia na mitazamo yao na vilevile kuboresha uelewaji wa mazingira yao (McCullis, na Chamberlain, 2013). Mwalimu **$MW_{22}KN$** alipozungumzia ndoa za lazima alisema yafuatayo:

> *Tamaduni potovu zilizopitwa na wakati zinachangia ndoa za lazima hasa kwa watotowa kike wanaolazimishiwa ndoa. HF ya **Ngome ya Nafsi** inaangazia haya kupitia Mzee Mengo ambaye aliamua kumwoza Naseko kwa Mzee Sakaja ili apate mahari. Hathamini masomo kwa wasichana. Baadhi ya watoto wa kike hupitia changamoto kama hizi na kunyimwa nafasi ya kuendeleza kisomo. Wao hulazimika kutafuta usaidizi kutoka kwa serikali au mashirika mengine.*

Kwa mujibu wa nukuu hii, ni wazi kwamba tamaduni potovu bado zimeshamiri katika jamii. Ndoa za lazima zimekuwa kikwazo kikubwa kwa wasichana, hali ambayo inakwaza maendeleo yao ya elimu. Baadhi ya wazazi hawathamini elimu ya mtoto wa kike bali huthamini mali kwa hivyo kwao kumpata mtoto msichana ni chanzo cha kutajirika. Iwapo BB itatumika katika ufundishaji wa fasihi, itakuwa nafuu kwa kuiga tamaduni ambazo ni chanya na kutupilia mbali zile ambazo ni hasi. Kulingana na BB, hadithi inafaa ilenge umri wa mwanafunzi, iweze kupokelewa na tamaduni mbalimbali. Waandalizi wa mitaala ya elimu wanaweza kuzingatia hadithi fupi ambazo zinatilia mkazo tamaduni ambazo hazijapitwa na wakati katika uteuzi wa vitabu vya kusoma hasa vya fasihi. Kauli hii pia inaashiria kwamba serikali ina jukumu la kutekeleza hasa kumlinda mtoto wa kike dhidi ya tamaduni potovu. Hili limewekwa wazi katika katiba ya Kenya 2010 ambapo ndoa za mapema na za lazima zimepingwa. Hata hivyo, ni wajibu wa serikali kufuatilia hili na kulitekeleza bayana.

Umaskini ni tatizo ambalo huathiri baadhi ya wanafunzi shuleni. Wao hukosa mahitaji yao ya kila siku. Taswira hii imejitokeza katika baadhi ya HF. Mwalimu **$MW_{7}KI$** alisema yafuatayo:

> *Kuna baadhi ya wanafunzi ambao hupitia hali kama ile ya Mashaka katika HF ya Ndoto **ya Mashaka.** Alifiwa na wazazi kisha akalelewa na Biti Kidebe lakini katika hali ya umaskini. Analazimika kufanya kazi za mshahara duni ili kujikimu kimaisha. Wanafunzi wengine wanaotoka katika tabaka la kimaskini hulazimika kufanya kazi duni ili kuweza kujilipilia karo ya shule na kununua mahitaji mengine. Baadhi ya wanafunzi huishi katika mitaa duni kama ya Tandale alikoishi Mashaka.*

Naye mwalimu **$MW_{27}W$** akizungumzia tatizo la umaskini miongoni mwa wanafunzi alisema yafuatayo:

> *Mhusika Bogoa na wazazi wake katika HF ya **Tulipokutana Tena** wanaishi maisha ya kimaskini. Familia hii inakosa hata uwezo wa kifedha wa kununua sabuni. Bogoa alikuwa na shati moja pekee iliyompwaya*



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

> *mwilini. Kuna wanafunzi wanaopitia hali kama hii ya Bogoa ya kukosa mahitaji ya kimsingi kwa sababu ya umaskini. Hali hii inambidi Bogoa kuajiriwa na Bi Sinai mjini amfanyie kazi za nyumba.*

Umaskini unasawiri hali halisi katika maisha ya wanajamii. Visa vinavyoelezwa kupitia hadithi fupi hizi vinatoa taswira halisi ya matatizo wanayopitia baadhi ya wanafunzi. Manufaa ya usomaji kwa wanafunzi ni kama kuimarisha kujithamini, kuliwaza na kuwapa namna ya kuyakabili masuala tata kama vile umaskini (Goddard, 2011).Wanafunzi wanapozisoma hadithi fupi hizi hugundua kuwa wao si wa kwanza kupitia hali kama hii ya umaskini. Prater na wengine (2006) wanaamini kuwa ushauri wa kutumia vitabu unaweza kutumiwa kutoa maarifa ama ujuzi wa kuangalia shida na hivyo kusaidia mwanafunzi kupata suluhu ya matatizo. Stadi za kutatua matatizo pia zimeimarika miongoni mwa wanafunzi wenye ulemavu. Bibliotherapia hisia huwa na manufaa kwa wanafunzi kwa kuwa huwasaidia kutalii hisia na mapitio pamoja na fikira fiche kwa kutumia matini zenye visa ili kusaidia wanafunzi kuhusisha hisia na mazoea yao na yale ya wahusika. Licha ya kwamba BB imekisiwa kama mojawapo wa malengo katika silabasi ya fasihi nchini Kenya, waratibu wa mitalaa ya elimu hasa fasihi wanapaswa kuizingatia. Hii ni kwa sababu bibliotherapia inaweza kutambua kuwa mwanafunzi anayepitia tatizo fulani hayuko peke yake katika shida fulani. Hili litasaidia kuepuka hisia za upweke. Aidha, inasaidia kujifunza kuhusu suala linaloweza kumpa mtu maneno yafaayo na ukakamavu wa kutafuta usaidizi zaidi kama vile kuongea na marafiki, jamaa, walimu, waajiri na hata katika mahojiano. Bibliotherapia inasaidia wasomaji kupata maarifa mapya kuhusu masuala changamano wanayokabiliana nayo na namna ya kuyasuluhisha. Rosenblatt (1978) katika nadharia ya NMMM anakubaliana na maelezo haya anaposema hadhira hubashiri na kuyahusisha wayakutayo katika hadithi na yale aliyoshuhudia maishani.

Baadhi ya wanafunzi wa kike baada ya kupata mimba wasizotarajia huamua kuavya kama suluhu kwa tatizo hili. Uavyaji mimba huwa ni hatari kwa kuwa wengine huishia kuyapoteza maisha yao. Katika baadhi ya HF kuna wahusika wanaopitia tatizo hili. Mwalimu **MW₂KI** alisema yafuatayo:

> *Mimba zisizohitajika huwasukuma wanafunzi wa kike kutafuta suluhu kupitia Uavyaji. Taswira hii imejitokeza katika HF ya* ***Shogake Dada ana Ndevu.*** *Mhusikaalimwalika Kimwana nyumbani kwa kisingizio cha kudurusu vitabu kwa pamoja.*
> *Hatima yake ni Safia kuwa mjamzito na alipojaribu kuavya mimba ile aliaga dunia.*
> *Ni hatari wanafunzi kuamua kuavya mimba kwa kuwa wanaweza wakapoteza maisha yao. Kuna wanafunzi wanaokabiliwa na tatizo kama hili linalojitokeza katika hadithi fupi.*

Hata wanafunzi wa vyuo vikuu hukabiliwa na tatizo hili. Mhusika Christine katika HF ya ***Samaki wa Nchi za Joto*** ni mwanafunzi wa chuo kikuu lakini aliyapuuza masomo na kuingilia anasa. Mwisho wake alipata mimba na kuamua kuiavya. Aliyahatarisha maisha yake. Suluhu si uavyaji wa mimba afadhali kutafuta usaidizi kwa walimu au wazazi.

Ukosefu wa nidhamu miongoni mwa baadhi ya wanafunzi hasa wa shule za upili umeongezeka. Walimu pamoja na wazazi hutumia mikakati mbali mbali ili kuwasaidia wanafunzi hawa. Migomo shuleni husababishwa na ukosefu wa nidhamu.Suala hili limeangaziwa katika HF. Mwalimu MW26W alisema yafuatayo:

> *Ukosefu wa nidhamu huchangia kutokea kwa migomo shuleni. Wahusika Kamaliza na Mbunda katika HF ya Ndimi za Mauti waliamua*



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

> *kufanya mgomo katika shule yao ya Angeko. Hasara kubwa ilitokea pamoja na vifo vya wenzao. Wanafunzi hupitia hali kama hii hasa wanapojiunga na makundi ya wanafunzi wakosa adabu. Masuala ya ukosefu wa nidhamu yamesawiriwa katika hadithi fupi.*

Mifano hii iliangazia wazi kuwa hadithi zilimulika masuala yaliyowaathiri wanafunzi katika jamii. Masuala kama vile matumizi ya dawa za kulevya, ndoa za lazima, uavyaji mimba, ukosefu wa nidhamu, umaskini na mapenzi ya shuleni. Iwapo BB itatumika katika mtalaa wa elimu nchini Kenya, itawasaidia wanafunzi kudhibiti shida zao za kihisia bila kuingiliwa na wataalamu kwa kuwa vitabu ambavyo vitateuliwa na KICD vitapaswa vimulike yale yaliyopitiwa na watu walio na changamoto kama zao. Hivyo basi, usomaji wa hadithi hizi husaidia kupunguza ama kukomesha tatizo lililoko kabla ya kuwa tatizo sugu; na vilevile husaidia kujenga mambo mema na mabadiliko ya kimtazamo yanayosababishwa na tatizo fulani. Wanafunzi hawafai kufikiria wao ni wa kwanza kukumbwa na tatizo kama hilo. Kulingana na Rosenblatt (1995) matini ni kama kichocheo cha kuibua tajriba mbalimbali za zamani, fikira na mawazo kutoka kwa msomaji. Katika HF wanafunzi huweza kuibua tajriba zao za zamani. Usomaji wa HF zinazosawiri matatizo ya wanafunzi utawawezesha kutagusana na wahusika wanaozipitia hali kama zao. Kulingana na Aiex (1997), usomaji wa vitabu vya hadithi kwa mwanafunzi humfanya aone kwamba wahusika wengine wanakabiliana na matatizo sawa na yake na kwamba ni njia moja ya kuainisha majadiliano kuhusu matatizo ambayo mwanafunzi angesitasita kujadili. Hali hii inamsaidia kuweka huru shinikizo la hisia zinazojengeka ndani yake.

**b) Suluhu kwa Matatizo yaWanafunzi**

Maishani binadamu huweza kuwa na njia zaidi ya moja ya kutatua tatizo linalomkumba.Kibibliotherapia vitabu vya hadithi fupi vinapaswa kuonyesha jinsi wanafunzi wanaweza kutataua matatizo wanayopitia katika maisha. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa asilimia 36 ya walimu walikubali sana kuwa HF zinaonyesha wahusika wameweza kusuluhisha matatizo yao. Kauli hii ya mwalimu **$MW_{17}KA$** mmoja inathibitisha hili:

> *Katika hadithi fupi ya Kijembe cha Ngariba mhusika Clara alilazimishiwa tohara ili awe tayari kuozwa. Mhusika Clara kwa usaidizi wa shirika moja la Kimarekani alitoroshwa. Kutoroshwa kwake Clara kumsaidia kujiepusha na tohara na vilevile ndoa ya lazima. Anapata nafasi ya kuendelea na masomo yake.*

Naye mwalimu **$MW_{10}KA$** alisema yafuatayo;

> *Naseko katika hadithi fupi ya* ***Ngome ya Nafsi*** *alitoroka ndoa ya lazima na kwenda kwa makao ya watoto ya Bi Tesi ili kuendelea na masomo yake baada ya babake kutaka kumwoza kwa Mzee Sakaja.*

Wahusika Naseko na Clara walifanikiwa kutoroka mitego ya ndoa za lazima na kuendeleza masomo yao. Tamaduni potovu huwazuia wasichana kuendelea na masomo yao. Bibliotherapia inaweza kuwasaidia wanafunzi wote kujifunza namna ya kukabiliana na changamoto za kijamii na kihisia ambazo zinaweza kutokea (Maich na Kean, 2004). Kwa sababu katika jamii za kiafrika kuna tamaduni mbalimbali, Taasisi ya Ukuzaji Mitaala inapaswa kuteua vitabu vya hadithi ambavyo vinaangazia tamaduni ambazo ni chanya katika jamii na zile ambazo ni hasi kama


© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

vile tohara ya wasichana na ndoa za mapema hazipaswi kushirikishwa katika hadithi hizo. Fauka ya hayo, KICD inafaa izingatie vitabu vya fasihi ambavyo vimeandikwa na wakenya kutoka jamii mbalimbali. Hadithi ambazo zinaangazia mila na mahitaji ya wanafunzi kinafsia pamoja na namna ambavyo tamaduni mbovu hutokea zinapaswa kupewa nafasi katika mtalaa wa elimu hasa somo la fasihi. Hivyo basi, wanafunzi watajifunza kutokana na wahusika wa kibibliotherapia ambao ni sharti waweze kukabiliana na matatizo yanayowakumba maishani.

Hata hivyo data ya utafiti huu vilevile ilionyesha kuwa asilimia 64ya walimu walidai kuwa wahusika katika hadithi fupi walishindwa kupata suluhu kwa matatizo yao. Mwalimu **MW₂₆W** alisema yafuatayo:

> *Mhusika Sela katika hadithi ya* ***Kanda la Usufi*** *alishindwa kupata suluhu baada ya kujihusisha katika mapenzi akiwa shuleni na kupata mimba. Kwanza anakosa nafasi ya kurudi shuleni na anapojaribu kumtorosha mtoto wake alianguka mtoni na kufa maji.*

Hali kadhalika mwalimu ***MW₂₃KN*** alisema yafuatayo**:**

> *Samuel Matandiko katika HF ya Mtihani wa Maisha alipopokea taarifa kuwa ameanguka mtihani wa kidato cha nne aliamua kujitoa uhai kwa kujirusha mtoni ili afe. Hakustahili kujiua kwa sababu ya kufeli mtihani. Angetafuta njia mwafaka ya kujiendeleza kimaisha. Mtihani haufai kuwa kipimo cha kufaulu maishani.*

Mwalimu ***MW₃KI aliongezea*** yafuatayo:

> *Walimu wa Nanda katika HF ya* ***Fumbo la Mwana*** *waligundua alikuwa ameanza kushiriki uraibu wa dawa za kulevya. Hili linaathiri usafi na viwango vyake vya masomo. Hapati suluhu kwa tatizo hili ila mzazi alifahamishwa kuhusu hili.*

Mojawapo wa mhimili wa BB ni kwamba kitabu kilichoteuliwa kinahitaji kuwa na hadithi inayovutia na suluhu la tatizo linaloshughulikiwa lahitaji kuaminika pia. Katika HF hii mwandishi aliangazia athari za dawa za kulevya kwa wanafunzi wakiwa shuleni. Hatoi suluhu kupitia mhusika Nanda labda ni vipi angejiepusha na matumizi ya mihadarati. Mwanafunzi anaposoma hadithi kama hii anastahili kutagusana na mhusika na kuiga kusuluhisha matatizo yake jinsi afanyavyo mhusika. Hadithi ambazo hazitoi suluhu mwafaka kwa wanafunzi wanaokabiliwa na matatizo ya aina hii zinastahili kutathminiwa na KICD kabla ya kuteuliwa katika silabasi ili wanafunzi wasije wakaiga suluhu mbovu kuhusiana na tatizo fulani.

Mwalimu MW6KI alinena yafuatayo:

> *Mhusika Mashaka katika HF ya* ***Ndoto ya Mashaka*** *baada ya kufiwa na wazazi alilelewa na Bi Kidebe ambaye alikuwa maskini. Mashaka hapati suhulu ya kuepuka hali. Anaendelea kuishi katika mtaa duni na kufanya vibarua ili kujikimu. Anatorokwa na mke kwa sababu ya umaskini.*

Naye mwalimu **MW₁₆KA** anaonyesha jinsi mhusika Christine katika HF ya ***Samaki wa Nchi za Joto*** anashindwa kupata suluhu ya kupata utajiri. Anasema yafuatyo:

> *Christine alipuuza masomo yake ya chuo kikuu na kujiingiza katika anasa na starehe. Ana uhusiano wa kimapenzi na Mzungu kwa jina Mr. Peter kitarajia kupata mali. Badala yake alipata mimba na kuiavya.*

Mwalimu **MW₁₀KA** akizungumzia HF *ya* ***Mapenzi ya Kifaurongo*** anaonyesha jinsi Dennis alishindwa



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

kujikwamua kutoka hali yake ya umaskini. Alisema yafuatayo:

> *Mhusika Dennis ana uhusiano wa kimapenzi na Penina ambaye anatoka katika familia ya kitajiri. Waliamua kuoana matarajio ya Dennis yakiwa ni kujiondoa katika hali ya umaskini. Familia ya Dennis ilikuwa ya tabaka la chini. Penina aliamua kukatiza uhusiano wao.*

Kutokana na matini hizi ni wazi kwamba baadhi ya hadithi zinatoa suluhu ambazo hazifai kwa wanafunzi. Licha ya kwamba katika silabasi ya shule za sekondari nchini Kenya msisitizo upo katika kuchanganua maudhui, wahusika na mbinu za uandishi, taasisi ya elimu nchini inafaa kutathmini hadithi ambazo zinatoa suluhu hasi. Iwapo hadithi ambazo zimeteuliwa zitatoa suluhu mwafaka, wanafunzi wanaweza kuhisi nafuu kwamba wao si wa kwanza kukumbwa na tatizo hilo.Wao watajifunza kutatua matatizo yao na kutafakari juu ya jinsi wahusika katika kitabu hutatua yao. Long (2010) anakubaliana na haya anaposema kuwa bibliotherapia yafaa kumsaidia mtu kujali kuhusu hisia za mwenzake. Hivyo basi, msomaji hupunguza machungu na hasira ya kindani anapojitambulisha na mhusika katika fasihi. Hii ndiyo bibliotherapia ambayo KICD wanashauriwa kuzingatia wanapoteua vitabu vya fasihi vya kusomwa na wanafunzi wa shule za upili. Hadithi fupi zinazoweza kutumika kwa bibliotherapia zinafaa kuwasaidia wanafunzi kusuluhisha matatizo yao. Wanafunzi wanastahii kutagusana na mhusika katika hadithi na kuiga jinsi anavyokabiliana na changamoto zake. Walimu asilimia 36walipokubaliana kuwa wahusika katika hadithi fupi teule walipata suluhu kwa matatizo yao ni ishara kuwa hadithi hizo kwa kiasi zinaweza kutumika kwa bibliotherapia miongoni mwa wanafunzi. Mawazo haya yanaoana na yake Harbaugh (1984), aliyechunguza ufaafu wa BB katika kuwafunza wafungwa wachanga wa kike stadi mbalimbali za kushughulikia matatizo yanayowakabili ili wanapofunguliwa waweze kukubalika katika jamii. BB iliwafaa hawa wafungwa wa kike hata baada ya kumaliza kifungo chao. Walimu pia walikubaliana kuwa kusoma hadithi fupi huwasaidia wanafunzi kupata ufahamu mpya juu ya hali ngumu wanayokabiliana nayo. Katika suala hili, data ilionyesha kuwa asilimia 64ya walimu walidai kuwa wahusika wa HF hawakufanikiwa kusuluhisha matatizo yao. Kwa mujibu wa Maich na Kean, (2004) wahusika wa kibibliotherapia sharti waonyeshe mbinu za kukabiliana na shida na suluhu kwa matatizo yao.

Matokeo haya yanawiana na mapitio ya matini jinsi wengine walivyotaja kwamba kutumia fasihi kunaweza kusuluhisha masuala mbalimbali (Hynse, na Hynse-Berry, 2012 na Pardeck, 1994). Isitoshe, matokeo haya yalidokeza kwamba malengo mengine ya bibliotherapia yanaweza kukubalika katika mazingira ya darasani ilhali mada nyingine zinafaa kutumiwa katika mazingira ya hospitali. Katika malengo haya mawili, washiriki walionyesha kiwango cha chini cha ukubalifu wa kutekelezwa darasani. Hali hii iliwiana na maonyo ya wataalamu kwamba walimu watumie bibliotherapia kwa malengo ya ukuaji na sio kwa malengo ya kimatibabu. Kwa mujibu wa utafiti huu walimu waliamini kwamba baadhi ya masuala haya yanaweza kushughulikiwa kwenye bibliotherapia elimu au kuaji.

### c) Uaminifu wa Wahusika kwa Wanafunzi

Prater na wengine (2006) waliwapa walimu miongozo ya kutumia wanapoteua kazi za kifasihi za kutumika kwa BB darasani. Walipendekeza kwamba vitabu vinafaa kuteuliwa kwa misingi ya uhalisia na uaminifu wa wahusika kwa wanafunzi wanaovisoma vitabu hivyo. Wahusika katika hadithi hii wawe wanaweza kuaminika katika hali halisi ya kimaisha na waeleweke katika kiwango cha mwanafunzi.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa asilimia 79ya walimu walikubali kuwa wahusika wanaaminika. Mwalimu MW3KI akitoa maoni yake alisema yafuatayo:

> *Mhusika Nandako katika HF ya **Kipendacho Moyo ni Dawa** anaaminika kwa wanafunzi kwa kuwa ni mwanfunzi wa shule ya upili kama wao. Alifuzu mtihani wake wa kidato cha nne kwa Alama ya A. Familia yake ilikuwa ya kimaskini kama ya baadhi ya wanafunzi.*

Hali kadhalika mwalimu **MW$_8$KI** aliongezea yafuatayo:

> *Wahusika wanafunzi kama vile Naseko katika **Ngome ya Nafsi** na Clara katika **Kijembe cha Ngariba** wanaaminika miongoni mwa wanafunzi. Baadhi ya wanafunzi wamepitia hali kama zao za kupinga ndoa za lazima.*

Mwalimu MW10KA katika kuthibitisha uaminifu wa wahusika kwa wanafunzi alisema yafuatayo:

> *Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya limeongezeka miongoni mwa vijana. Hivyo Wanafunzi kukutana na mhusika Nanda katika Fumbo **la Mwana** wanamwamini. Athari za matumizi ya mihadarati inajitokeza wazi kupitia Nanda.*

Idadi ndogo ya walimu ambayo ni 14% walisema kuwa baadhi ya wahusika hawaaminiki na wanafunzi. Mwalimu **MW$_{20}$KA** alisema yafuatayo:

> *Hadithi kama **Samaki wa Nchi za Joto** inamzungumzia Christine ambaye ni mwanafunzi wa chuo kikuu anashiriki ulevi na mapenzi kiholela naye Peter ambaye ni Mzungu. Mwishowe alipata mimba na kugundua hayomapenzi hayakuwa ya dhati. Alipoteza muda wake bure. Si rahisi mwanafunzi wa shule ya upili kujihusisha na maisha ya chuo kikuu ambayo hana tajriba. Nayo Bibliotherapia haiwezi kuwepo.*

Matokeo ya walimu yalionyesha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi katika HF wanaaminika na kueleweka katika kiwango cha wanafunzi wa shule za upili. Matini inayoteuliwa kutumika kwa BB lazima iwe na wahusika wanaoaminika na wanafunzi (Cook na wenzake, 2006). Wahusika kama hawa wanaweza kutumika kwa BB kwa sababu wanafunzi hujitambulisha na kutagusana nao kwa urahisi. Ikiwa mwanafunzi atashindwa kujitambulisha na wahusika katika hadithi au apoteze hamu ya kukisoma kitabu hicho, basi hataweza kungamua maana ya hadithi hiyo na mwishowe kitabu kitakosa kufikia malengo ya kutoa mtakaso na kumpa nafuu (Kavanaugh na Fiorini, 2009). Matokeo kuhusu wahusika wa hadithi fupi yanaonyesha umuhimu wa wahusika katika kuathiri tabia ya mwanafunzi. Zaidi ya hayo, matokeo yanaonyesha umuhimu wa wahusika katika kufanikisha bibliotherapia kupitia kwa mahusiano na wasomaji. Hivyo basi, KICD inafaa ishirikishe vyuo vikuu pamoja na walimu kutafiti ili wateue vitabu mwafaka kwa wanafunzi kwa kuzingatia umri, uwezo wa kusoma, maudhui yanayojitokeza na usawiri wa wahusika wanaopitia matatizo yaliyo sawa na yale ya wanafunzi husika.

### d) Kujithamini kwa Wanafunzi

Mtafiti kupitia hojaji alitaka kujua maoni ya walimu hasa ikiwa HF inampa mwanafunzi uwezo wa kujithamini au hapana.Walimu asilimia 93walikubaliana sana kuwa wanafunzi wanaweza kujithamini ilihali asilimia 7ya walimu walikataa. Kauli ya mwalimu **MW$_{23}$KN** inathibitisha yafuatayo:



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

> *Tamaduni potovu huwafanya watoto wa kike kutojithamini lakini kupitia baadhi hadithi fupi kuna watoto wa kike wanaojithamini kama vile Naseko katika* ***Ngome ya Nafsi*** *na Clara katika* ***Kijembe cha Ngariba*** *walipotoroka ndoa ya lazima na kuendelea na masomo yake.*

Hali kadhalika **MW27W *alisema*** yafuatayo:

> *Jamii ya Mtondo kaskazini katika hadithi ya* ***Uteuzi wa Moyoni*** *haikuwathamini watoto wa kike walipofika darasa la nne walilazimika kuozwa. Hata hivyo mhusika Zena alikaidi hayo alipotoka katika ndoa ya lazima na kujiendeleza kimasomo na hatimaye kugombea kiti cha ubunge cha eneo hilo. Zena alikuwa mfano wakuigwa na wanafunzi.*

Wahusika Naseko na Clara wanajithamini kwa kukwepa ndoa za lazima na kuendeleza masomo yao. Msimamo wao thabiti unawasaidia kupinga tamaduni potovu katika jamii zao. Hawa ni wahusika wakuigwa na wanafunzi wanapozisoma hadithi hizi fupi. Mfano mwingine ni Zena ambaye anatoka katika ndoa ya mateso na kuamua kujiendeleza kimasomo na kisha kugombea kiti cha ubunge. Katika bibliotherapia wanafunzi wanaposoma hizi hadithi fupi hutagusana na wahusika hivyo kujifunza jinsi ya kujithamini maishani. Wanafunzi kutagusana na wahusika huwasaidia kujifunza mengi kupitia kwa hawa wahusika. Kwa mujibu wa Prater na wenzake (2005) walimu wanaweza kuwasaidia watoto au vijana kutumia bibliotherapia kupitia viwango vitatu ambavyo ni: kujitambulisha, mtakaso-hisia na umaizi. Wanafunzi wanapotagusana na wahusika katika fasihi huwa ndio kiwango cha kwanza ambacho ni cha utambulisho. Mwanafunzi hujitambulisha na mhusika ambaye anapitia changamoto kama zake maishani. Mwanafunzi hivyo huweza kuzielewa tabia za kibinadamu. Matokeo ya kijumla yanahusu uimarishaji wa kujithamini, kuboreka kwa stadi za kukabili mambo, kujitambua, kujieleza, kutambua suluhisho la matatizo, kuvumilia matatizo, uwezo wa kuratibu mazoea ili kuyaelewa zaidi, uwezo wa kufanya maamuzi na kutafakari (Montgomery na Maunders, 2015).

Mwalimu wa shule ya kaunti ndogo MW22KN alionyesha jinsi Bogoa anajithamini alisema yafuatayo:

> *Bogoa katika HF ya* ***Tulipokutana Tena*** *alipelekwa kwa Bi Sinai mjini kwenda kumfanyia kazi za kinyumbani. Bi Sinai alimtesa kwa sababu alikuwa ametoka katika familia ya kimaskini. Aliamua kutoroka ili kujiepusha na mateso hayo ingawa alikuwa maskini. Alijithamini ndio sababu akachukua hatua hiyo.*

Hali kadhalika mwalimu **MW25W** akizungumzia HF ya ***Mame Bakari*** alisema yafuatayo:

> *Ubakaji wa Sara unamwathiri hadi aliogopa kuwafahamisha wazazi wake kwa kuhofia angefukuzwa nyumbani kwao. Kinyume na matarajio babake anamkubali na kumtania Mame Bakari. Ingawa alikuwa amehofia mwanzoni lakini mwishowe anajithamini wazazi walipomkubali. Wazazi wana jukumu la kuwahimiza watoto wao kujithamini maishani.*

Mhusika Bogoa anatoroka kwa Bi Sinai ili kujiepusha na mateso pale nyumbani ni kutokana na kujithamini kwake. Mwalimu **MW25W** anaonyesha jinsi wazazi wake Sara wanamkubali baada ya kubakwa na kupata mimba. Sara anajithamini baada ya wazazi kumkubali. Baada ya kuzisoma hadithi kama hizi wanafunzi wanaweza kuwaiga wahusika kama hawa. Hadithi fupi ambazo zina wanafunzi wanaojithamini ina sifa za kibibliotherapia.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Taasisi ya KICD wanashauriwa kuviteua vitabu ambavyo vina wahusika wanaojithamini. Hata hivyo ingawa asilimia 93ya walimu waliunga mkono kuwa wahusika katika HF hujithamini waliobaki 7% walipinga wazo hili kuonyesha kuwa wanafunzi hawajithamini. Mwalimu MW5KI alisema yafuatayo:

> *Samuel Matandiko katika HF ya* ***Mtihani wa Maisha*** *baada ya kuanguka Mtihani wa kidato cha nne alikata tamaa ya kuishi na kujitosa katika bwawa ili afe. Kukosa matumaini maishani ni njia moja ya kutojithamini.*

Naye mwalimu **$MW_{27}W$** katika HF ya ***Mapenzi ya Kifaurongo*** alisema yafuatyo:

> *Dennis alikata tamaa alipofukuzwa na mpenzi wake Penina kutoka nyumba walikoishi katika mtaa wa New Zealand kwa sababu kutoka katika familia ya kimaskini. Penina alimtaka Dennis amtafute mchumba mwenye hali kama yake. Hali hii inamfanya Dennis kutojithamini.*

Katika bibliotherapia wanafunzi wanaposoma hizi hadithi fupi hutagusana na wahusika hivyo kuwaiga. Hadithi fupi zilizo na wahusika wasiojithamini kama Samuel hazistahili kwa matumizi ya BB. Mwalimu **$MW_5KI$** anaonyesha jinsi Samuel anakata tamaa na kutaka kujiua kwa sababu ya kufeli mtihani wa kidato cha nne. Kifo hakifai kuwa suluhu kwa mwanafunzi aliyefeli mtihani. Mwanafunzi kama huyu anakosa kujithamini. Samuel si mhusika kielelezo. Dennis naye anakosa kujithamini kwa sababu ya mvutano wa kitabaka kati yake na mpenzi wake Penina ambaye amekulia katika familia ya kitajiri. Hivyo basi KICD wangefaa kuzingatia suala la BB katika mtalaa wa elimu hasa wakati huu taifa lina mjadala wa kubadilisha mtalaa wa elimu. Jambo hili litasaidia walimu wabadili jinsi wanavyofunza hadithi fupi kama vile wanafunzi kushiriki katika majadiliano ya kimakundi na shughuli za kufuatiza kama vile kuandika jarida ili msomaji aweze kujielewa, ajithamini na kuboresha namna anavyofanya maamuzi ya kibinafsi na ya kijamii. Vitabu vya fasihi vinavyoteuliwa kusomwa na wanafunzi katika shule za upili nchini Kenya vinastahili kuwa na wahusika vielelezo. Kavanaugh na Fiorini (2009) wanakubaliana na mawazo haya kuwa kuwa kitabu kilichoteuliwa kwa usomaji wa wanafunzi shuleni kinahitaji kuwa na hadithi inayovutia na mhusika mkuu awe kielelezo bora.

### e) Kubadili Mitazamo ya Wanafunzi Kimaisha

Mtafiti kupitia walimu alitaka kujua ikiwa HF inaweza kubadilisha mitazamo ya wanafunzi. Data hii ilionyesha walimu kushuku ikiwa mitazamo ya wanafunzi kuhusu maisha iliathiriwa na wao kuzisoma hadithi fupi. Kwa hoja hii asilimia 36 ya walimu walikubali sana na waliobaki asilimia 64walipinga. Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi wengi hawabadili mitazamo yao baada ya kusoma hadithi badala yake wao hupata mafunzo kupitia hadithi hiyo. Kauli za walimu zinathibitisha kuwa mitazamo ya wanafunzi haibadiliki wanapozisoma hadithi fupi. Mwalimu ***$MW_5KI$*** alisema yafuatayo:

> *Wanafunzi wanapozisoma hadithi fupi haibadilishi mitazamo yao badala yake wao hupata mafunzo. Kwa mfano wanaposoma hadithi fupi ya* ***Fumbo la Mwana*** *mitazamo yao haibadiliki bali wao hujifunza kujiepusha na matumizi ya mihadarati.*

Hali kadhalika mwalimu MW10KA alitoa kauli ifuatayo:

> *Wanafunzi wengi hujifunza maadili kutokana na hadithi fupi. Kwa mfano Katika hadithi ya* ***Samaki wa Nchi za Joto*** *wanajifunza kujiepusha na anasa na Starehe*



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

> *badala yake kuzingatia masomo. Hadithi fupi zinatoa mafunzo waliyojifunza wanafunzi bali sio mabadiliko ya kimawazo. Wanafunzi wanaposoma HF ya* ***Ndimi za Mauti hawabadili*** *mtazamo wao ila wanajifunza kujiepusha na migomo shuleni.*

Mwalimu wa shule ya wilaya **MW$_{26}$W** akirejelea HF ya ***Shogaake Dada ana Ndevu*** alisema yafuatayo:

> *Mwanafunzi anaposoma hii hadithi anapata mafunzo kuwa uongo haufai. Maisha ya Safia yalifikia mwisho kwa kuavya mimba aliyoipata kupitia kuwahadaa wazazi wake alipokuwa akitembelewa na Shogaake Kimwana aliyekuwa na Ndevu. Mwishowe Safia kukosa kuendelea na masomo yake. Haya mafunzo ni muhimu kwa wanafunzi wote. Wazingatie masomo na wajiepushe mapenzi wakiwa shuleni na kwamba uavyaji mimba ni hatari huenda wakapoteza maisha yako. Hata hivyo mtazamo wa haubadiliki.*

Data ya utafiti huu ilionyesha kuwa asilimia 64ya walimu walidhihirisha kuwa HF hazina uwezo wa kubadili mtazamo wa wanafunzi ila hutoa mafunzo ya kuwasaidia maishani. Mwalimu **MW$_{5}$KI** anaeleza kuwa wanafunzi wanapozisoma hadithi fupi haibadilishi mitazamo yao badala yake wao hupata mafunzo. Kwa mfano kuweza kjiepusha na matumizi ya mihadarati kupitia **HF** ya ***Fumbo la Mwana***. Hali kadhalika mwalimu **MW$_{10}$KA** anathibitisha haya kwa kusema kuwa wanafunzi wengi hujifunza maadili kutokana na hadithi fupi. Usomaji wa HF hauwezi kumbadilisha msomaji kimtazamo bali itabidi apate matitabu kumsaidia kupambana na matumizi ya mihadarati. Hili hutilia shaka matumizi ya hadithi kama hii kwa BB. Idadi kubwa za HF zilishindwa kutimiza hili hivyo kutilia shaka matumizi yake kwa BB. Kwa hivyo, KICD inashauriwa kuteua vitabu vya fasihi ambavyo vina uwezo wa kubadili mtazamo wa mwanafunzi hii itakuwa kielelezo cha kwanza kuwa hadithi fupi ina athari ya kibibliotherapia kwa msomaji. Chambers (1990) anasisitiza kuwa nadharia ya mapatano ya mwitikio wa msomaji (NMMM) inapendekeza kuwa mtunzi anajenga uhusiano na msomaji ili aweze kugundua maana ya matini. Kwa hivyo asili ya fasihi inafaa kutazamwa kama sanaa ya kutendwa ambapo kila msomaji anajenga utendaji wake wa kipekee unaohusiana na matini. Kwa mkabala huu, utafiti ulilenga kuchunguza athari ambazo hadithi fupi zinaweza kuwa nazo kwa mwanafunzi na mtazamo wake. Kilicho wazi katika matokeo hayo ni kwamba wanafunzi wanajifunza mafunzo muhimu kupitia mtagusano wao na wahusika katika hadithi fupi.

Hata hivyo, matokeo ya utafiti yalithibitisha kuwa 36% ya walimu ndio walikubali kuwa kuna HF chache ambazo zina uwezo wa kubadili mtazamo wa wanafunzi wanapozisoma. Mwalimu **MW$_{12}$KA** alisema yafuatayo:

> *Clara katika hadithi ya* ***Kijembe cha Ngariba*** *anatafuta usaidizi wakati mila potovu za kupashwa tohara zinapolazimishwa na wazazi. Clara alibahatika kupata shirika linalomtorosha hadi ng'ambo ili aendeleze masomo yake. Mtazamo wa wanafunzi unabadilika kuhusu imani kuwa mahala pa Mwanamke ni jikoni.*

Naye mwalimu **MW$_{3}$KI** alisema yafuatayo:

> *Usomaji wa HF ya* ***Mtihani wa Maisha*** *unabadilisha mtazamo wa mwanafunzi kuhusu kufeli mitihani. Huo si mwisho wa maisha anavyofanya Samuel Matandiko kutaka kujitoa uhai alipojiangusha bwawani baada ya kufeli mtihani wa kidato cha nne.*



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Utafiti huu ulibainisha asilimia 36ya walimu walionyesha uwezekano wa HF kubadili mtazamo wa mwanafunzi. Mwalimu **$MW_{12}KA$** anaonyesha jinsi mwanafunzi anaweza kubadili mtazamo wake kuhusu imani kuwa mwanamke mahala pake ni jikoni hasa baada ya kuisoma **HF** ya ***Kijembe Cha Ngariba***. Anaonyesha jinsi Clara anatoroka kuozwa anagli mchanga na badala yake kuijiendeleza kimasomo. Naye mwalimu **$MW_{3}KI$** anaangazia jinsi kufeli mtihani sio mwisho wa maisha. Usomaji wa HF ya ***Mtihani wa Maisha*** unabadilisha mtazamo wa mwanafunzi kuhusu kufeli mitihani. Kuadilika kwa mtazamo wa mwanafunzi ni ishara kuwa HF hizi zinaweza kutumika kwa BB. Matokeo haya yanashadidia anayosema Atwood (1982) akisisitiza dhima ya NMMM, aliposema kuwa kitendo cha usomaji ni mfanyiko unaombadilisha msomaji na hawezi kuwa mtu yule aliyekuwa kabla na baada ya kuisoma matini. NMMM ina ile nadharia ya mapatano ya mwitikio wa msomaji ya (Rosenblatt, 1995). Hata hivyo, matokeo haya yanafichua udhaifu wa wanafunzi kuhakiki nafasi za wahusika na athari zao kwa maisha yao. Zaidi ya hayo uwezo wa wanafunzi wa kubadili mtazamo kupitia kujitambulisha na wahusika hivyo basi unatiliwa shaka.

**f) Kuigwa kwa Wahusika na Wanafunzi**

Mtafiti kupitia walimu alitaka kujua ikiwa HF ina wahusika wa kuigwa na wanafunzi.

Matokeo ya utafiti kutokana na hojaji yalionyesha asilimia 75% ya walimu walikubaliana kuwa HF zina wahusika wanaoweza kuigwa na wanafunzi shuleni ilihali asilimia 25 walipinga haya. Mwalimu **$MW_{6}KI$** alikubaliana na kauli hii aliposema:

> *Wahusika katika hadithi fupi wanaweza kuigwa na wanafunzi. Naseko katika hadithi ya* ***Ngome ya Nafsi*** *ni mhusika aliye na msimamo thabiti kwa kuwa alipinga ndoa ya lazima anayolazimishiwa na babake. Huyu ni mhusika wa kuigwa na wanafunzi hasa wa kike.*

Naye mwalimu **$MW_{10}KI$** alisema yafuatayo:

> *Mhusika Mzee Mago katika hadithi ya* ***Tumbo Lisiloshiba*** *amewajibika alipowatetea wachochole dhidi ya kunyanganywa shamba lao na matajiri kwa fidia ndogo. Wanafunzi wanaweza kuiga kuwajibika katika jamii na hata shuleni.*

Mhusika Abu katika HF ya **Ndoa ya Samani** ni mfano mzuri wa kuigwa na wanafunzi. Mwalimu **$MW_{27}W$** alisisitiza haya aliposema yafuatayo:

> *Abu alikuwa ni mwenye bidii na asiyekata tamaa. Mwanzoni alifanya kazi za kijungu jiko lakini baadaye alipata kazi ya uhamali Uarabuni na akafanya kazi kwa bidii ya mchwa. Bidii hii ni ya kuigwa na wanafunzi.*

Kulingana na kauli hizi za asilimia 75 walimu walithibitisha kuwa kuwa HF nyingi zina wahusika wa kuigwa ambao wanaweza kuwa vielelezo kwa wanafunzi hivyo kuonyesha ufaafu wa HF kwa BB. Mwalimu **$MW_{6}KI$** alieleza jinsi mhusika Naseko anakaidi tamaduni potovu ili kukwepa ndoa ya lazima na mapema ili aweze kuendelea na masomo yake. Tayari babake alitaka kumwoza kwa Mzee Sakaja. Ana msimamo thabiti hivyo ni mhusika wakuigwa na wanafunzi. Hali kadhalika mwalimu **$MW_{27}W$** anaonyesha jinsi mhusika Abu katika ***Ndoa ya Samani*** ana bidii mithili ya mchwa. Bidii hii ni ya kuigwa na wanafunzi masomoni. HF hizi zinaweza kutumika kwa BB. Kavanaugh na Fiorini (2009) miongoni mwa wengine wamependekeza kuwa kitabu kilichoteuliwa kutumika kwa BB kinahitaji kuwa na mhusika mkuu ambaye ni kielelezo bora kwa wanafunzi. Wanafunzi wanapojitambulisha na mhusika katika hadithi na wasiweze kutagusana naye mchakato wa kibibliotherapia hauwezi kujitokeza.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

ISSN: 2663-9289

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Ingawa asilimia 75 ya walimu walithibitisha kuwa wahusika wa HF wanaweza kuigwa kuna asilimia 25 waliopinga hili. Mwalimu mmoja wa shule ya wilaya **$MW_{27}W$** alisema yafuatayo:

> *Baadhi ya wahusika hawawezi kuigwa kwa kuwa wamepotoka kimaadili. Kamaliza katika hadithi ya* ***Ndimi za Mauti*** *aliposhirikiana na wenzake Kuanzisha mgomo katika shule ya Angeko na kusababisha vifo vya wanafunzi wenzao kwa kulichoma bweni. Huu ni ukosefu wa nidhamu. Wanafunzi hawafai kuiga vitendo kama hivi.*

Naye mwalimu ***MW4KI*** *alisema* yafuatayo:

> *Bi Sinai hawezi kuigwa kwa kuwa katika hadithi ya* ***Tulipokutana Tena*** *alimtumikisha Bogoa mtoto wa miaka mitano na kumnyima nafasi ya kwenda shuleni. Anamfanyisha kazi za kufagia, kufua na kuchanja kuni. Anadai mtoto wa kimaskini hastahili kwenda shuleni. Huyu si mhusika wa kuigwa. Anastahili kuwa mtetezi wa mtoto huyu.*

Walimu **$MW_{12}KN$, $MW_{9}KI$ na $MW_{26}W$** walieleza jinsi mhusika Samuel Matandiko katika hadithi ya ***Mtihani wa Maisha*** hawezi kuigwa na wanafunzi kwa kuwa aliamua kujitoa uhai baada ya kuanguka mtihani wa kidato cha nne. Wanafunzi hawastahili kukata tamaa maishani hata baada ya kufeli mtihani. Kujiua si suluhu kwa tatizo hili.

Mwalimu **$MW_{14}KA$** akizungumzia HF ya ***Kachukua Hatua Nyingine*** alisema yafuatayo:
Taasisi ya mitaala ya KICD inastahili kuteua hadithi fupi zilizo na wahusika wanaoweza kuigwa na wanafunzi ili kuwasaidia kusuluhisha changamoto zao. Pia silabasi inafaa izingatie masuala ya bibliotherapia sio tu uchanganuzi wa maudhui na wahusika. Matokeo haya yalionyesha kwamba walimu waliamini kwamba kutumia matini ya fasihi darasani kunaweza kusaidia kufanikisha bibliotherapia kwa wanafunzi wanaokumbana na migogoro. Matokeo haya yanakubaliana na maoni ya Aiex (1997) kwamba usomaji wa vitabu vya hadithi kwa mwanafunzi humfanya aone kwamba wahusika wengine wanakabiliana na matatizo sawa na yake. Matokeo haya yanaonyesha ukubalifu wa kutumia bibliotherapia kwa wanahirimu darasani kushughulikia malengo mbalimbali.

### i) Usawa wa Kijinsia

Kavanaugh na Fiorini (2009) wamependekeza kuwa kitabu kilichoteuliwa kwa matumizi ya BB kinahitaji kuwa na hadithi ambayo itapokelewa na tamaduni mbalimbali huku ikizingatia usawa wa kijinsia. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa asilimia 86ya walimu walikubalina kuwa HF zina wahusika wanao onyesha usawa wa kijinsia ilhali asilimia 24walipinga hili.
Mwalimu **$MW_{5}KI$** *alisema yafuatayo:*

> *Katika HF ya* ***Kanda la Usufi*** *kuna usawa wa kijinsia. Mwandishi amewasawiri Sela na Masazu ambao ni wanafunzi wa shule ya upili. Wana uhusiano wa kimapenzi unaosababisha Sela kuwa mjamzito na kuacha shule.*

Naye mwalimu **$MW_{27}W$** akizungumzia HF ya ***Samaki wa Nchi za Joto*** alisema yafuatayo**:** *Wahusika wa jinsia zote wamesawiriwa katika hadithi hii. Christine na Zac ni wanafunzi wa chuo kikuu cha Makerere. Hawazingatii masomo ila wanajihusisha kwa anasa na starehe.*
Mwalimu **$MW_{10}KA$** alisema yafuatayo:

> *Katika HF ya* ***Damu Nyeusi*** *mwandishi amesawiri wahusika wa jinsia zote. Fikirini na msichana mmoja wa Kimarekani ni wanafunzi wa chuo kikuu huko Marekani.*



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

**Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)**

**ISSN: 2663-9289**

**DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228**
**Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|**
**Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org**
**Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal***

*Msichana wa Kimarekani alishirikiana na kakaake kumwibia Fikirini na hata kumbagua kwa sababu yeye ni Mwafrika.*

Hata hivyo usawa wa kijinsia unakosekana wakati waandishi wanawasawiri wahusika wa jinsia ya kiume kwa mtazamo hasi. Mwalimu **$MW_6KI$** alisema yafuatayo:

*Mhusika Nanda katika HF ya **Fumbo la Mwana** anasawiriwa kwa matazamo hasi kama mpenda mihadarati. Anashindwa kumudu masomo shuleni na hata viwango vya usafi.*

Naye mwalimu **$MW_{10}KI$** akizungumzia HF ya ***Mtihani wa Maisha*** alitoa kauli ifuatayo:

*Samuel Matandiko ni mhusika wa kiume anasawiriwa kwa mtazamo hasi kama mhusika aliyekata tamaa na kukosa matumaini maishani hasa alipoamua kujitoa uhai baada ya kufeli mtihani*

.

Mwalimu **$MW_{22}KI$** wa shule ya kaunti ndogo akirejelea HF ya ***Ndimi za Mauti*** alisema yafuatayo*:*

*Mwandishi aliwasawiri wahusika wa jinsia ya kiume kuwa waanzilishi wa mgomo katika Shule ya Angeko. Wana wachomea wanafunzi wenzao katika bweni.Uharibifu wa mali nyingi unatokea. Kamaliza na wenzao walisawiriwa kama wakatili na wakosa utu.*

Kauli za walimu zinadhihirisha wazi kwamba suala la jinsia linazingatiwa katika hadithi fupi. Hata hivyo, kuna baadhi ya hadithi ambazo zinasawiri jinsia ya kiume kwa njia potovu. Iwapo wanafunzi wa kiume watasawiriwa kama walevi, wabakaji, wenye kufeli mitahani basi wanafunzi hawa wanaweza kuwa na mfadhaiko katika masomo yao. Kwa mujibu wa mwongozo wa Maich na Kean, (2004) hadithi inayoweza kutumiwa kwa BB sharti isawiri usawa wa kijinsia. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa asilimia 86ya walimu walionyesha kuwa hadithi fupi zimesawiri usawa wa kijinsia. Hata hivyo asilimia 24ya walimu walipinga hili. Kuna baadhi ya waandishi ambao wamewasawiri wahusika wa kiume kwa mtazamo hasi. Nanda katika **HF** ya ***Fumbo la Mwana*** amesawiriwa kama mhusika aliyeathiriwa na mihadarati kiafya na kimasomo ilhali katika jamii kuna watoto wa kike ambao wameathirika kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Samuel Matandiko katika HF ya ***Mtihani wa Maisha*** alikata tamaa baada ya kufeli mtihani wa kidato na kuamua kujitoa uhai anashindwa kupata suluhu kwa tatizo lake. Hii si hali halisi katika jamii kwa kuwa watoto wa kike vilevile hukata tamaa baada ya kuanguka mitihani. Mgomo unaotokea katika shule ya Angeko katika HF ya ***Ndimi za Mauti*** umeongozwa na watoto wa kiume. Kamaliza na wenzake wanasababisha hasara kubwa ya mali na hata vifo vya wenzao. Migomo haiongozwi na wavulana pekee kuna wasichana ambao pia hushiriki. Wahusika ambao wamesawiriwa kwa mtazamo hasi ni nadra kutumika kwa BB. Mawazo ya Kavanaugh na Fiorini (2009) miongoni mwa wengine yanathibitisha kuwa kitabu kilichoteuliwa kinahitaji kuwa na hadithi inayovutia na tatizo na suluhisho linaloshughulikiwa lahitaji kuaminika pia mhusika mkuu awe kielelezo bora. Mwanafunzi asifadhaishwe na kuumizwa na mambo fulani katika kitabu hicho na aweze kujitambulisha na mhusika mkuu; hadithi ilenge umri wa mwanafunzi na iweze kupokelewa na tamaduni mbalimbali huku ikizingatia usawa wa kijinsia. Sifa hizi zitatoa mwelekeo kwa KICD na walimu wanapoteua vitabu vya kusomwa na wanafunzi wake.

### j) Ufaafu kwa Umri wa Wanafunzi

Mawazo ya Kavanaugh na Fiorini (2009) miongoni mwa wengine wanapendekeza kuwa kitabu kilichoteuliwa kinahitaji kuwa na hadithi inayovutia na ilenge umri wa mwanafunzi. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa



**© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org**

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228

ISSN: 2663-9289

Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|

Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org

Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

asilimia 68ya walimu walikubali kuwa HF zinalenga umri wa wanafunzi ilhali asilimia 32walidai kuwa baadhi ya HF hazilengi umri wa wanafunzi.

Mwalimu **MW$_5$KI** alisema yafuatayo:

> *Mwandishi wa hadithi fupi ya **Kanda la Usufi** amewasawiri Sela na Masazu ambao walipokutana walikuwa wanafunzi wa shule ya upili. Walianza uhusiano wa kimapenzi na kusababisha Sela kupata mimba. Wahusika hawa ni wa umri sawa na wanafunzi wanaoisoma hadithi hii hivyo basi kutagusana na hawa wahusika itakuwa rahisi.*

Naye mwalimu wa shule ya kaunti **MW$_{16}$KA** akizungumzia HF *ya* ***Kipendacho Moyo ni Dawa*** alitoa kauli ifuatayo:

> *Nandako ni mwanafunzi ambaye tayari amefuzu mtihani wa kidato cha nne na kufuzu kwa Alama A na asubiri kuingia chuo kikuu. Hii ni hadithi ambayo imelenga hasa umri wa wanafunzi walio shuleni. Maudhui ya elimu hapa pia yanawalenga wanafunzi.*

Mwalimu **MW$_{28}$W** alisema yafuatayo:

> *Hadithi ya **Ndimi za Mauti** inazungumzia migomo ya wanafunzi shuleni. Kamaliza na wenzake kupanga mgomo katika shule yao. Wanafunzi wa shule za upili hushiriki migomo. Hii inalenga yale wanayopitia katika umri wao.*

Mwalimu **MW$_{23}$KN** katika hadithi ya ***Mkimbizi*** alitoa kauli ifuatayo:

> *Msimulizi katika hadithi hii ni mwanafunzi ambaye ni mkimbizi aliyetorokea usalama kwa nchi jirani. Kwa bahati nzuri anapata nafasi ya kuendeleza kisomo chake kule Marekani. Kuna wanafunzi wa umri kama wake ambao wanapitia hali hii. Hadithi hii imelenga umri wa wanafunzi.*

Naye mwalimu **MW$_7$KI** alisema yafuatayo:

> *Safia katika hadithi fupi ya **Shogake Dada ana ndevu** aliwahadaa wazazi wake kumbe alikuwa akimwalika mpenzi wake nyumbani kwao. Visa kama hivi huwaathiri wanafunzi walio shuleni. Hadithi hii inawatosheleza wanafunzi kiumri.*

Ingawa hadithi hizi zinawalenga wanafunzi kiumri asilimia 28ya walimu walipinga hili. Mwalimu **MW$_{27}$W** alitoa kauli ifuatayo:

> *Hadithi zinazozungumzia wanafunzi wa vyuo vikuu hazilengi umri wa hawa wanafunzi kwa mfano hadithi za **Samaki wa Nchi za Joto** na **Damu Nyeusi** zimewalenga wanafunzi walio katika vyuo vikuu ilhali hawa ni wa shule za msingi.*

Naye mwalimu **MW$_6$K**I alisema yafuatayo:

> *Hadithi inayosawiri wanandoa hailengi umri wa wanafunzi walio shuleni. Hadithi ya **Mke Wangu** inalenga mgogoro wa kindoa ulioko kati ya Msimulizi na mkewe Aziza. Hadithi hii huenda isiwafae wanafunzi wa shule za upili.*

Baadhi ya hadithi huzingatia suala la umri wa wanafunzi katika wahusika wanaotumiwa. Licha ya kwamba mtalaa wa elimu nchini Kenya hasa kuhusiana na fasihi haujazingatia hali hii katika silabasi, vitabu vya hadithi vinavyoteuliwa vinapaswa kulenga umri wa wanafunzi. Hadithi inayopaswa kutumika kwa BB sharti ilenge wanafunzi kiumri. Hili litawawezesha wanafunzi kutagusana na wahusika ambao ni wa umri sawa na wao. Wanafunzi watajitambulisha kwa urahisi na wahusika walio shuleni kama wao kwa mfano Sela na Masazu. Hata hivyo, huenda BB isitendeke ikiwa wanafunzi watashindwa kutagusana na wahusika ambao ni wana ndoa na vilevile wanafunzi wa vyuo vikuu. Wanafunzi darasani watahitaji kutengewa shughuli mbali mbali



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)
ISSN: 2663-9289
DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, Double –Blind Peer Reviewed Journal

wakati wa kusoma kitabu ili kuwawezesha huona mwingiliano kati yao na wahusika wa hadithi. Ni rahisi mwanafunzi kutagusana na mhusika katika hadithi fupi ikiwa mhusika huyu ana umri sawa naye (Kokesh, na Sternadori, 2015).

## HITIMISHO

Matokeo ya mitazamo ya walimu kuhusu ufaafu wa HF kufanikisha BB kwa wanafunzi ilionyesha kuwa asilimia 100 ya walimu walikubali kuwa HF huangazia matatizo yanayowakabili wahusika kwa hivyo kuwezesha matini kutumika kwa BB. Wahusika waliosawiriwa katika HF waliaminika na kuweza kuigwa na wanafunzi. Wahusika katika HF waliweza kujithamini na kusawiriwa kwa usawa wa kijinsia na kulenga umri wa wanafunzi. Hata hivyo Wahusika walishindwa kupata suluhu kwa matatizo yao hivyo kukwaza BB huku wanafunzi wakikosa kubadili mitazamo yao na badala yake kupata mafunzo kupitia usomaji wa HF hizi. Matokeo haya yalidhihirisha kufaulu kwa kiasi kwa hadithi fupi kama njia ya kufanikisha bibliotherapia pengine kwa sababu wahusika katika matini ya hadithi fupi hawakuzwi vizuri na waandishi kwa sababu ya ufupi wa utanzu wenyewe. Takwimu zimeonyesha mahusiano ambayo inaashiria mahusiano ya kiwango cha chini kati ya wahusika katika hadithi fupi na uwezo wao wa kufanikisha bibliotherapia kwa wanafunzi kwa sababu ya wahusika kushindwa kupata suluhu kwa shida zao. Wahusika kuweza kupata suluhu ndicho kiini kikuu cha BB kwa kuwa mtagusano na mhusika hujitokeza kupitia mtakaso hisia kati ya msomaji na mhusika wa HF. Matokeo haya yalionyesha kuwa wanafunzi wa hadithi fupi za Kiswahili wana uwezo mkubwa wa kufaidika zaidi kupitia kwa kujihusisha na maudhui kuliko wahusika katika hadithi fupi.

## MAREJELEO

Aiex, N. K. (1997). *Bibliotherapy*. Bloomington; Indiana University office of Educational Research and Improvement.

Atwood, M. (1982). *Second Words* Toronto. House of Anansis Press.

Chambers, A. (1990). *The Reader in the Book*. In Peter Hunt (Ed) *Children's Literature*: *The Development of Criticism*. Routledge 91-113.

Cook, K. E, T, & Ganz, J. B. (2006). *Bibliotherapy. Intervention in School* and *Clinic*, 42(2), 91-100. https://doi.org/10.1177/10534512060420020801.

Doss, P. G. (2010). *The Effect of Classroom Bibliotherapeutic Intervention on Perceptions of Bullying among Teachers of Young Children Aged Four and Five* (Doctoral dissertation). https://digitalcommons.kennesaw.edu/etd/415.

Dawn, E. M. (2020). *A Case Study, Teachers' Perceptions of Read-Aloud Bibliotherapy in the Classroom* (Unpublished doctoral dissertation). Grand Canyon University Phoenix.

Forgan, J. W. (2002). *Using Bibliotherapy to Teach Problem-Solving Intervention in School and Clinic* (75-82).

Goddard, A. T. (2011). 'Children's books for use in bibliotherapy'. In *Journal of Pediatric Health Care,* 25(1), 57–61.

Harbaugh, J. K. (1984). *The Effectiveness of Bibliotherapy in Teaching Problem-Solving Skills to Female Juvenile Deliquents.* Drake University.

Kavanaugh, C. A., & Fiorini, J. J. (2009). 'Uses of Bibliotherapy for adoptive children and their families'.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Paper presented in *The American Counseling Association Annual*

Kokesh, J., & Sternadori, M. (2015). The good, the bad and the ugly: A qualitative study of how young adult fiction affects identity construction'In Atlantic *Journal of Communication,* 23(3), 139-158.

Lutovac, S., & Kaasila, R. (2011). 'Beginning a pre-service teacher's mathematical identity work through narrative rehabilitation and bibliotherapy'. In *Teaching in Higher Education,* 16(2), 225-236.

Maich, K. & Kean. S. (2004). 'Read two books and write me in the Morning: Bibliotherapy for Social Emotional Intervention in the inclusive Classroom.' In *Teaching Exceptional Children Plus*., 1, 5.

McCulliss, D. (2012). 'Bibliotherapy: Historical and research perspectives'. In *Journal of Poetry Therapy,* 25(1), 23–38.

McCulliss, D., & Chamberlain, D. (2013). Bibliotherapy for youth and adolescents: School-based application and research. Journal *of Poetry Therapy: The Interdisciplinary Journal of Practice, Theory, Research, and Education,* 26(1), 13–40.

Montgomery, P., & Maunders, K. (2015). 'The effectiveness of creative bibliotherapy for internalizing, externalizing, and prosocial behaviors in children: A systematic review'.In Children *and Youth Services Review,* 55, 37–47.

Prater, M. A., Johnstun, M. L., Dyches, T. T., & Johnstun, M. (2006). *Using Books as Bibliotherapy for at Risk Students: A Guide for Teachers. In Creating Inclusive Classrooms: Effective and Reflective Practice.* Pearson/Merrill Prentice. University of Virginia

Rosenblatt, L. (1995). *Literature as Exploration* (5th ed.). The Modern Language Association of American.

Rozalski, M. (2010). Bibliotherapy: Helping children cope with life's challenges. In *Kappa Delta Pi Record,* 47(1), 33-37.

Stewart, P. E., & Ames, G. P. (2014). 'Using culturally affirming, therapeutically appropriate bibliotherapy to cope with trauma'. In Journal *of Child and Adolescent Trauma, 7,* 227–236.

Turner, J. C. (2006). Representations of illness, injury, and health in children's picture books. Children's Health Care 35(2), 179-189.

Walibora, K., & Mohammed, S. A (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*. Nairobi: Maximillan Publishers Ltd.

Walibora, K. & Mohammed S.A. (2007). *Kiti cha Moyoni na Hadithi nyingine*. Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2004). (Mha): *Mayai Waziri wa Maradhi.* Focus Publishers.

Wilson, S. (2014). "Fail at maths and you fail at life": Learned barriers to equal opportunities - Mathematics anxiety and quality of life. In P. Brown & R. Faragher (Eds.). *Quality of Life and Intellectual Disability: Knowledge Application to Other Social and Educational Challenges*. Nova Press.

Wilson, S., Lyons, T., & Quinn, F. (2013). 'Should I stay or should I go?' Rural and remote students in first year university STEM courses. *Australian and International Journal of Rural Education, 23*(2), 77-88.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org

Editon Consortium Publishing
Transforming Scholarly Publishing

Editon Consortium Journal of Kiswahili (ECJKISW)

DOI: 10.51317/ecjkisw.v3i1.228
ISSN: 2663-9289
Volume: 03 Issue: 01 | June-2021|
Received: 08.05.2021; Accepted 10.05.2021; Published on 05.06.2021 at www.editoncpublishing.org
Mavisi, R. et al., *Editon Cons. J. Kiswahili.*, *Double –Blind Peer Reviewed Journal*

Dobyns, K. (2015). *Increasing awareness and acceptance of children with disabilities through children's picture books*. Rocky Mountain University of Health Professions. http://doi.org/10.13140/RG.2.2.16906.16322

Hynes, A. M., & Hynes-Berry, M. (2012). *Biblio/Poetry therapy—the interactive process: A handbook* (3rd ed.). North Star Press of St. Cloud, Inc.

Pardeck, J. T. (1994). Using literature to help adolescents cope with problems. *Adolescence,* 29(114)*,* 421-427.

Long, S. M. (2010). Exploring Web 2.0: The Impact of Digital Communications Technologies on Youth Relationships and Sociability. http://scholar.oxy.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1001&context=sociology

Chokocho. C. & Kayanda.D. (2016). (Mha). *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.* Longhorn Publishers.



© 2021, Editon Consortium Publishing | This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Non Commercial-Share Alike 4.0 International License. | Website: www.editoncpublishing.org